

Ulemavu nchini Marekani



Nchini Marekani, watu walio na ulemavu wanajumuishwa kwenye shule, kazi na jamii.

Ulemavu hauchukuliwi kuwa tukio baya wala kushindwa kibinafsi.

Wamarekani wengi walio na ulemavu huishi maisha huru na yenye mafanikio.

Vuguvugu la Haki za Ulemavu Marekani

Wamarekani walio na ulemavu wamepigania haki ya kuheshimiwa na kujumuishwa.

Wamesaidia kuunda sheria za kujumuishwa katika shule, usafiri wa umma, mpango ya serikali, makao na zaidi.



Haki za Kisheria

Wamarekani walio na ulemavu wana haki ya:

- Kuenda shuleni;
- Kuishi na kufanya kazi kwenye jamii yao;
- Kutembelea biashara za umma;
- Kutetea mahitaji yao;
- Kushiriki kikamilifu katika jamii.

Je, mtoto wangu akiwa na ulemavu?

Ikiwa unafikiri kuwa mtoto wako ana ulemavu, **usisubiri kumpeleka shuleni.**

Watoto wote nchini Marekani wana haki ya kuenda shuleni. Mtoto wako anaweza kupokea usaidizi shuleni.



Huenda likawa jambo la kutisha au kukanganya kugundua kuwa mtoto wako ana ulemavu, lakini kuna huduma nyingi katika jamii na shule yako. Kwa maelezo zaidi kuhusu huduma, tazama kipeperushi *Ni Nani Ninayeweza Kuwasiliana Naye kwa Usaidizi wa Elimu Maalum kwa Mtoto Wangu?*



Beyond Flight
ARIZONA MY HOME
Along the path of freedom lie the seeds of hope

Mpango wa Makao kwa Wakimbizi wa Arizona
1789 West Jefferson
Phoenix,
Arizona 85007
Simu: (602) 542-6045